

KARIBU KUJIUNGA NA CHEKECHEA

Kufunza Matumizi ya Choo



Kufunza matumizi ya choo huenda ikawa mada tata kwa familia za watoto wachanga. Kila mtoto hujisimamia katika matumizi ya choo kwa kasi tofauti. Familia yako inaweza kutumia mbinu zinazofaa zaidi katika kumsaidia mtoto wenu kufikia lengo la kujisimamia katika matumizi ya choo. Watoto wanapoingia shule ya chekechea, walimu na wafanyakazi wako tayari kuwakaribisha watoto jinsi walivyo. Hii inajumuisha kuwafunza kutumia choo!

Shuleni, watoto watajaribu kutumia choo bila usaidizi. Haijalishi iwapo mtoto wako amefunzwa kikamilifu jinsi ya kutumia choo au la, kuna vipengele vya kutumia choo ambavyo anaweza kuanza kujifanyia. Pitia orodha ifuatayo na mtoto wako. Fanya mazoezi ya stadi ambazo mtoto wako bado hawezi kujifanyia.



Ndiyo	Stadi za Kujisimamia katika Matumizi ya Choo
	Ninaweza kumuita mtu mzima ninapohitaji kutumia choo.
	Ninaweza kujivua na kujivisha suruali ninapotumia choo.
	Ikiwa nitatumia msala, ninaweza kuteremsha suruali yangu vya kutosha kutumia choo bila kufichua sehemu ya chini ya mwili wangu.
	Ninaweza kutumia karatasi shashi kujipangusa.
	Ninaweza kusuuza choo.
	Ninaweza kunawa mikono.

Kwa Wazazi

Mazingatio kwa Mpito wa Watoto kwenye Chekechea

- Mvishe mtoto wako nguo ambazo ni rahisi kwake kuteremsha na kuvuta juu.
- Eleza mahitaji ya mtoto wako katika kutumia choo kwa mwalimu wake wa chekechea. Walimu wanaweza kumsaidia mtoto wako kuweka na kufikia malengo wakati wanatumia choo shuleni.
- Hakikisha kuna chupi na nguo za ziada kwenye begi la mtoto wako iwapo 'ajali' itatokea.
- Iwapo mtoto wako ana mahitaji ya kiafya yanayohusiana na matumizi ya choo, zungumza na mtoa huduma ya afya au mtaalamu anayemshughulikia mtoto wako. Wanaweza kujaza fomu ili kusaidia shule kuunda mpango wa kushughulikia mahitaji haya.

Vidokezo kwa Ufunzaji wa Kutumia Choo

- Mpongeze mtoto wako anapojaribu kutumia choo, hata kama atapatwa na 'ajali'. Unapofanya hivi, hatakuwa na wasiwasi kuhusu mchakato huo.
- Fanya mpango. Mfanye mtoto wako ajaribu kwenda chooni anapoamka asubuhi na baada ya kulala mchana, kabla ya kutoka nyumbani, kabla ya kulala mchana au usiku, na kabla ya kula chakula.
- Tumia [rasilimali kutoka JCPS Early Childhood](#) ili ujifunze zaidi kuhusu ufunzaji wa matumizi ya choo. Inajumuisha chati ya kufuatilia wakati mtoto wako anafaulu katika sehemu ya mafunzo ya kutumia choo.